TOLEO LA 29

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb,

Tunapoendelea kusherehekea kufunguliwa upya kwa majengo yetu, na kujirekebisha kwa masomo mahuluti, ni ngumu kupuuza kile kilichotokea katika jimbo letu na kote nchini. Kama watu wengi, nimesikitishwa sana na matukio mabaya ambayo yalifanyika tarehe 16 Machi katika Atlanta na Kaunti ya Cherokee. Ongezeko la vurugu na chuki dhidi ya watu halikubaliki na haliwezi kuruhusiwa. Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) inasimama dhidi ya aina zote za chuki, ubaguzi wa rangi na vurugu, na tunaungana na jamii ya Waasia na watu wa asili ya Visiwa vya Pasifiki.

Wilaya yetu ya shule inajumuisha watu wa aina mbalimbali, na tunasherehekea utofauti huu kwa kila njia. Hatufai kusahau sifa hii muhimu kwa sababu ya vitendo vya wachache. Kama jinsi Dk. Martin Luther King Jr. alisema, "Ukosefu wa haki popote ni tishio kwa haki kila mahali." Usalama na ustawi wa kihisia wa wanafunzi na wafanyakazi wote wa DCSD utabaki kuwa kipaumbele.

Chanjo na Upimaji wa COVID-19

Tunafurahi kutangaza kuwa Bodi ya Afya ya DeKalb (BOH) itakuwa mwenyeji wa Kliniki ya Chanjo kwa wafanyakazi mnamo tarehe 20 Machi, katika Shule ya Upili ya Elizabeth Andrews. BOH inaweza kutoa chanjo kwa waalimu na wafanyakazi takriban 1,250 katika tukio hili. Wafanyakazi wanaombwa wajiandikishe kwa tukio hili kwa kutumia anwani yao ya barua pepe ya "dekalbschoolsga.org", ikiwezekana. Kwa kuwa hili ni tukio la faragha kwa DCSD pekee, tunataka kuhakikisha kuwa watu wengine wanaostahiki hawatajiandikisha kwa tukio hili. Tafadhali angalia barua pepe yako ya wilaya kwa maagizo zaidi kuhusu jinsi ya kujiandikisha.

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb imeshirikiana na Vituo vya Upimaji wa COVID wa Bila Malipo ili kutoa vipimo vya COVID-19 kwa wafanyakazi na familia. Upimaji utapatikana kwa waalimu na wafanyakazi katika siku za Jumatatu, Jumanne na Jumatano katika Shule ya Upili ya Cross Keys kuanzia 11 asubuhi hadi 5 jioni; na siku za Jumanne, Jumatano na Alhamisi katika Shule ya Kati ya Bethune kuanzia 7 asubuhi hadi 1 mchana.

Ratiba itaendelea hadi mwisho wa muhula wa shule. Ili kuweka miadi, tafadhali tembelea www.freecovidtesting.us.  Chagua ‘Quick Registration’ ili upange miadi yako na uchague eneo la shule.

## Siku ya Kuwa Nje

Nilikuwa na mkutano mzuri na viongozi wa Eneo la IV (Region IV) kwa Siku ya Kuwa Nje ya DCSD. Nilikuwa na fursa ya kukutana na timu ya uongozi wa Shule ya Msingi ya Stone Mountain, kufuatilia mafundisho ya kikundi kidogo katika Shule ya Msingi ya Indian Creek na kutembelea kwa njia ya mtandaoni mkutano wa Mpango wa Hatua ya Muda Mfupi (STAP) katika Shule ya Kati ya Champion Theme.

Eneo la IV linafanya kazi nzuri ya kuweka malengo na kuhakikisha elimu bora kwa wasomi wetu wote. Ningependa kumshukuru Msimamizi wa Elimu wa Eneo Dk. Antonette Campbell kwa kujitolea kwake katika kuwasaidia wasomi wetu.

## Kifurushi cha Milo Iliyogandishwa ya Siku 7

Wanafunzi wote wa DCSD, walio na miaka 18 kwenda chini, sasa wanaweza kupokea vifurushi vya milo iliyogandishwa ya siku 7 iliyo na matunda na mboga. Usambazaji wa milo hufanyika siku za Jumatano kuanzia 11 asubuhi hadi 2 mchana. Kwa maelezo zaidi, bofya hapa.

## Mpango wa Masomo ya Msimu wa Kiangazi wa MOSAIC

Nina furaha kutangaza kwamba Wilaya itatoa mpango mpya wa masomo kwa wanafunzi katika msimu huu wa kiangazi. Mpango wa Masomo ya Msimu wa Kiangazi wa MOSAIC unatoa fursa za ziada za masomo ili kushughulikia upungufu wa masomo na upotezaji wa masomo. Mpango wa MOSAIC unajumuisha ujuzi wa msingi wa kusoma na kuandika na hisabati, ufahamu wa lugha, ufidiaji wa alama au upataji wa alama kwa haraka, STEM/STEAM, mpango wa ufidiaji wa msimu wa kiangazi na kambi za uboreshaji. Mitaala imeundwa kwa hali bora za masomo mnamo Juni na Julai 2021 na ili kuwapa wanafunzi usaidizi wa makusudi, unaolengwa ili kushughulikia mapungufu ya masomo.

Mipango hailipishwi, hata hivyo, ikiwa mwanafunzi wa shule ya upili atafanya kozi kupitia Georgia Virtual School au taasisi nyingine iliyothibitishwa, kuna ada kwa kila kozi. Wilaya inawahimiza wanafunzi wote kutumia fursa ya mpango ulioundwa kwa ajili ya kujiboresha.

Maelezo zaidi yatatolewa baadaye.

## Ukumbi wa Maelezo

Ningependa kuwashukuru wazazi na walimu wetu ambao walitazama na kushiriki katika ukumbi wetu wa maelezo wa mtandaoni wa hivi majuzi. Tunakushukuru kwa maoni na uzingatiaji wako wakati tunatoa maelezo kuhusu mpango wa kufungua

upya wa wilaya. Ikiwa ulikosa mkutano wa ukumbi wa maelezo, tafadhali bofya hapa ili kutazama.

Baraza la Ushauri la Jamii la Msimamizi wa Elimu

Ningependa kuwashukuru washirika wetu wa jamii na Baraza la Ushauri la Jamii ya Msimamizi wa Elimu (SCAC) kwa kukutana na timu yetu wiki hii. Wito wa SCAC ni kutoa usaidizi, mwongozo, na uongozi kwa msimamizi wa elimu kuhusiana na maswala ya ustawi wa kimasomo, utendaji na kifedha wa wilaya.

Ushirikiano huu ni muhimu kwa wilaya. Ushiriki wa jamii miongoni mwa wadau wote ni muhimu kwa mafanikio ya wilaya ya shule.

Mchango wa Zana za COVID-19

Ningependa kukishukuru Chama cha Mawakala wa Shamba cha DeKalb (Association of REALTORS) kwa msaada wake wa ukarimu kwa Shule ya Msingi ya Peachcrest. Shirika lilitoa mchango wa zana 50 za COVID-19 kwa waalimu katika juhudi za kuwasaidia kudumisha madarasa safi na salama. Zana zilijumuisha karatasi za kupangusa ili kutakasa, sanitaiza za mikono, barakoa za uso, ngao za uso na bidhaa za Lysol. Chama cha Mawakala wa Shamba cha DeKalb kimeshirikiana na DCSD kwa miaka kadhaa, na tunashukuru kwa ushirikiano huo.

Natumai kwamba sisi kama jamii tunaendelea kutendeana kwa wema na kuwapo kwa kila mmoja tunapopambana ili kumaliza janga hili la ulimwengu na athari za baadaye zinazowezekana.

Wako mwaminifu,

Bi. Cheryl Watson-Harris